



## **LESENI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA**

### **TAARIFA KWA UMMA**

BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA TANZANIA (GAMING BOARD OF TANZANIA) IMEBAINI KUWEPO KWA MKANGANYIKO JUU YA UTOAJI WA LESENI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA NCHINI. HIVI KARIBUNI BAADHI YA MAMLAKA ZIMEKUWA ZIKIJIHUSISHA NA UTOAJI LESENI/VIBALI VYA KUENDESHEA SHUGHULI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA BILA KUZINGATIA SHERIA YA MICHEZO YA KUBAHATISHA (GAMING ACT NO. 4 OF 2003). TUNAPENDA KUUFHAMISHA UMMA KUWA LESENI/VIBALI VYA KUENDESHEA SHUGHULI ZA MICHEZO YA KUBAHATISHA HUTOLEWA NA GAMING BOARD OF TANZANIA BAADA YA MWOMBAJI KUKIDHI VIGEZO VILIVYOAINISHWA KISHERIA IKIWA NI PAMOJA NA KUFANYIWA UPEKUZI WA KINA (BACKGROUND CHECK). MAREKEBISHO YA SHERIA YA LESENI (BUSINESS LICENSING ACT NO. 25 OF 1972) YALIYOFANYIKA MWAKA 2003 KUPITIA FINANCE ACT NO. 15 YA MWAKA 2003, KIFUNGU 5(1)(F), YALIONDOA MICHEZO YA KUBAHATISHA KATIKA ORODHA YA UHITAJI WA LESENI ZA BIASHARA, ISIPOKUWA LESENI INAYOTOLEWA NA GAMING BOARD.

LENGO LA TAARIFA HII NI KUONDOA UTATA UNAOJITOKEZA MARA KWA MARA KATI YA WAENDESHAJI NA BAADHI YA MAAFISA BIASHARA NA MAAFISA UTAMADUNI SEHEMU MBALIMBALI NCHINI. UTATA HUU KWA KIASI KIKUBWA UMEATHIRI SEKTA YA MICHEZO YA KUBAHATISHA NCHINI NA HIVYO KUIKOSHESHA SERIKALI MAPATO.

IMETOLEWA NA:

**KAIMU MKURUGENZI MKUU**  
**BODI YA MICHEZO YA KUBAHATISHA**  
**PO BOX 1717 DAR ES SALAAM, SIMU: 022 2124703/4**  
**EMAIL: [info@gamingboard.go.tz](mailto:info@gamingboard.go.tz)**